

2.3 Shughuli Zilizotekelezwa 2023 - 2024

Katika kipindi cha 2023-2024 Halmashauri ya Wilaya ya Pangani imeweza kutekeleza shughuli za mbalimbali za kimaendeleo kikiwa ni pamoja na;

- i. Ununuzi wa vifaa tiba katika kituo cha afya Mkalamo na Madanga vyenye thamani ya TZS. 300,000,000.00
- ii. Ununuzi wa vifaa tiba katika zahanati za Mkwaja, Kipumbwi, Kwakibuyu, Stahabu, Langoni, Kimang'a, Masaika na Kigurusimba vyenye thamani ya TZS. 100,000,000.00.
- iii. Ukamilishaji wa zahanati ya Mseko na Buyuni kwa gharama ya TZS. 100,000,000 ambapo zahanati ya Mseko imekamilika na Buyuni hatua za ukamilishaji.
- iv. Ujenzi wa nyumba ya walimu 2 kwa 1 shule ya sekondari ya Jumaa Aweso kwa thamani ya TZS. 98,000,000.00 ambayo tayari imekamilika.
- v. Ukamilishaji wa chumba 01 cha maabara sekondari ya Jumaa Aweso kwa gharama ya TZS. 30,000,000.00 ikiwa tayari imekamilika na inatumika.
- vi. Ukamilishaji wa vyumba 04 vya madarasa shule ya sekondari Jumaa Aweso kwa gharama ya TZS. 50,000,000.00 na kwas asa yamekamilika na yanatumika.
- vii. Ukamilishaji wa chumba 01 cha darasa shule ya msingi Kipumbwi kwa gharama ya TZS. 12,500,000.00 ambapo darasa limekwisha kamilika na linatumika.
- viii. Ukarabati wa vyumba 14 vya madrasa katika shule za msingi za Boza, Kipumbwi, Langoni, Mikinguni, Mtango, Mzambarauni na ujenzi wa darasa 01 shule ya msingi Mwembeni kwa gharama ya TZS. 180,000,000.00. Ukarabati huu na ujenzi umekamilika na madarasa yanatumika.
- ix. Ujenzi wa bweni 01 la wanafunzi wenye mahitaji maalum shule ya msingi Funguni kwa gharama ya TZS. 128,000,000.00. Ujenzi huu kwa sasa umefikia hatua za ukamilishaji ambao unahitaji fedha za nyongeza ili kukamilisha ujenzi.

- x. Ujenzi wa vyumba 08 vya madarasa na vyoo matundu 14 kwa ajili wanafunzi wa kidato cha tano na sita katika shule ya sekondari ya Bushiri na Funguni. Miradi hii imeakamilika ujenzi bado uwekaji wa viti na meza katika madarasa kwa shule ya sekondari Bushiri shughuli ambayo inaendelea. Miradi hii imegharimu TZS. 232,000,000.00
- xi. Ukamilishaji wa vyumba 08 na vyoo matundu 30 shule ya sekondari Pangani Halisi kwa gharama ya TZS. 116,000,000.00. Madarasa yamekamiliika na yanatumika, vyoo vya wasichana vimekamiliika na wavulana hatua za mwisho za ukamilishaji.
- xii. Ujenzi wa mradi wa Usafi kupitia SRWSSP katika zahanati ya Kigurusimba, Kituo cha afya Mkalamo, kituo cha afya Mwera, zahanati ya Mtango, Mtonga, Masaika, Kimang'a, Kipumbwi na Bushiri kwa gharama ya TZS. 375,756,000.00.
- xiii. Ujenzi wa mradi wa Usafi kupitia SRWSSP katika shule za msingi za Kimang'a, Makorora, Mtango na Tungamaa kwa gharama ya TZS. 189,326,546.66.
- xiv. Ukamilishaji wa mabweni 02 sekondari ya Tongani na Mwera kwa gharama ya TZS. 50,123,026.80 na
- xv. Ujenzi wa nyumba 01 ya Afisa Ugani Kilimo kata ya Masaika kwa gharama ya TZS. 40,000,000.00 ambayo ipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji.
- xvi. Ujenzi wa mabweni 02, vyumba 05 vya madarasa, choo cha matundu 08 kupitia BARRICK kwa gharama ya TZS. 401,800,000.00. Ujenzi huu kwas asa umesimama ukiwa katika hatua mbalimbali za ujenzi.